

SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbiqambo@gmail.com



MWONGOZO W A KILIMO CHA TANGAWIZI



SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com

TANGAWIZI

1.0UTANGULIZI:

Jina la kitaalamu ni **Zingiber officinale**

Tangawizi ni aina ya zao la kiungo ambalo sehemu inayotumika ni tunguu (rhizome) ambalo huonekana kama mizizi ya mmea. Asili ya zao hili ni maeneo ya kitropiki ya bara la Asia na hasa katika nchi za India na China. Zao hili linazalishwa kwa wingi kutoka katika nchi ya Jamaica. Hapa nchini zao hili hulimwa katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Morogoro, Pwani, Mbeya ,Kilimanjaro na Ruvuma – Madaba (Namtumbo na maeneo ya Songea vijijini tayari majaribio yanaoesha kustawi kwa zao hili



SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbiqambo@gmail.com

2.0 AINA ZA TANGAWIZI

Hakuna uthibitisho wa aina za tangawizi ambazo hulimwa hapa nchini ila kuna dalili ya kuwa na aina za White Africa (Jamaica) na Cochin (flint); hii huwa na tunguu ngumu zenye nyuzi



3.0 TABIA YA MMEA

Tangawizi ni mmea unaotambaa chini ya ardhi, wakati wa masika hutoa majani juu ya ardhi. Jamaica ina rangi hafifu ya kahawia na tunguu fupi wakati Cochin ina tunguu fupi zaidi lenye ngozi ya rangi iliyo kati ya kijivu na nyekundu. Mmea una urefu wa futi mbili na majani yake ni membamba marefu ambayo hufa kila mwaka yakiacha tunguu ardhini likiwa hai. Maua ya mmea huu yana rangi nyeupe au manjano.



SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com

4.0 HALI YA HEWA NA UDONGO

Zao hili hustawi katika maeneo yenye hali ya kitropiki, kutoka usawa wa bahari hadi mwinuko wa mita 1,500 au zaidi. Huhitaji mvua kiasi cha mm.1200-1800 na joto la wastani wa nyuzi za sentigredi 20-25. Hustawi vema katika udongo tifutifu wenye rutuba na usiotuamisha maji. Joto la wastani wa nyuzi 20c-24c huota vizuri. Hustawi vyema katika udongo wenye tifutifu na usiotuamisha maji

MMEA WA TANGAWIZI

5.0 UPANDAJI

Zao la tangawizi hupandwa kwa kutumia vipande vya tunguu vyenye kichipukizi kizuri angalau kimoja na huweza kukatwa katika urefu wa sm.2.5-5. Wakati mwingine, vichipukizi vinavyopatikana katika



kumenya tangawizi huweza kuhifadhiwa na kutumika kwa kupanda. Kiasi cha kilo 840-1700 cha vipande vya tunguu huweza kutumika kwa kupanda katika hekta moja, ama tani 1sawa na Kgs. 1000. Nafasi inayotumika kupanda ni kati ya sentimita.23-30 kwa 15-23 na kina cha sentimita.5-10 na mara nyingi hupandwa katika sesa. Baadhi ya mazao huweza kupandwa katika shamba la tangawizi ili kuweka kivuli chepesi ingawa si lazima kivuli kiwepo. Inashauriwa kumwagilia maji endapo mvua inakosekana.

SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com



Wiki 1-2 kabla ya kupanda weka mbolea ya samadi au mboji kiasi cha tani 25-30 kwa hekta na kwa maeneo ambayo hayana rutuba; inashauriwa shamba jipya au ambalo limekaa kwa muda wa miaka 2 au zaidi, kwa kuzingatia KILIMO HAI, amabacho kina soko kubwa; Tandaza nyasi shambani kuhifadhi unyevunyevu hasa pale kivuli kinapokosekana. Palizi hufanywa mara magugu yanapoota, dawa ya kuua magugu, kama simazine au round up hutumika.

6.0 MAGONJWA NA WADUDU:

- Madoa ya majani yanayosababishwa na viini vya magonjwa viitwavyo *Colletotrichum zingiberis* na *Phyllosticta zingiberi*.
- Kuoza kwa tunguu; kunasababishwa na viini viitwavyo *Pithium spp*
- Mizizi fundo; inasababishwa na *Meloidegyne spp*.



7.0 UVUNAJI

Tangawizi huweza kuwa tayari kwa kuvuna kati ya miezi 9-10 baada ya kupanda,

SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbiqambo@gmail.com

wakati majani yake yanapogeuka rangi kuwa njano na mashina kusinyaa. Tangawizi inayohitajika kwa kuhifadhi kwenye kemikali (preserved ginger in brine) huvunwa kabla haijakomaa kabisa, wakati ile iliyokomaa kabisa huwa kali zaidi na huwa na nyuzi hivyo hufaa kwa kukausha na kusaga. Mavuno hutofautiana kulinganana na huduma ya zao, mavuno yanaweza kuwa kiasi cha tani 10-30 cha tangawizi mbichi huweza kupatikana, kwa eka.



8.0 USINDIKAJI

Tangawizi ikisindikwa utapata unga, mafuta maalum (essential oils) n.k. Tangawizi iliyovunwa huweza kumenywa, kukatwa na kukaushwa juani au mara nyingine huchovywa katika maji yaliyochemka kwanza na ndipo kukaushwa au hukamuliwa mafuta. Pia tangawizi husindikwa na kuhifadhiwa kwenye chupa zikiwa zimechanganywa na sukari na/au chumvi au bila kuweka kitu chochote. Hata hivyo tangawizi ina Kiasi cha mafuta cha 16.0-18.0%.



SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com

9.0 SOKO LA TANGAWIZI

Soko la tangawizi lipo ndani na nje ya nchi, kiasi kikubwa kinauzwa nchini. Bei yake ni kati sh. 1,000-2,800/- kutegemeana na msimu.



10.0 GHARAMA ZA UZALISHAJI NA MAPATO GHARAMA YA HEKTA MOJA:

S/N0	HUDUMA	@ EKARI	KIWANGO	THAMANI
1	KUKODI SHAMBA	1	250,000	250,000
2	MBEGU	1	Kg.1000x 1500	1,500,000
3	VIBARUA	1	Mkataba	2,000,000
4	USIMAMIZI	1	Nyinginezo	1.600,000
	JUMLA YA GHARAMA			5,350,000

MAPATO kwa ekari moja kwa kipindi cha miezi 6-9	
Eka moja hutoa Tani 10 sawa na 10,000x Bei 1500	15,000,000

Kwa hesabu hiyo rahisi, inathibitisha kuwa Tangawizi, ni zao linalofuta gharama na kuwa lenye tija, kwa kuhusisha mazao mengine

SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com

11. ZIJUE FAIDA YA KUTUMIA TANGAWIZI:



Hutibu Magonjwa gani ?

Tangawizi husaidia yafuatayo:

- Kuongeza hamu ya kula
- Kupunguza kichefuchefu
- Kutapika, kuharisha
- Kisukari
- Shinikizo la damu
- Kuongeza msukumo wa damu
- Kutoa sumu mwilini
- Maumivu ya tumbo na
- Gesi tumboni.

Pia husaidia uyeyushwaji wa chakula tumboni. Vilevile husaidia wakati wa matatizo ya mafua au flu na magonjwa mengine mengi.

Kama utakuwa makini au kuwahi kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI basi magonjwa hayo hapo juu ni kati ya Magonjwa nyemelezi yanao wasumbua sana

SONGEA BUSINESS CLINIC COMPANY LTD.

P.O.Box 248, Songea

Reg. NO: 128839

Mobile phone: +255756096291,+255765599200,+255712421264

Email: songeabusinessclinic@gmail.com, ladslausbigambo@gmail.com

hawa ndugu zetu hivyo wakitumia Tangawizi basi wataweza kuondokana kabisa na matatizo hayo na kuishi vizuri na kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuepukana na kulala tu kitandani.

FURAHIA LADHA YA TANGAWIZI KWA AFYA YAKO



Copy right

@

Songea Business Clinic Co. Ltd 2016